Microsoft

# Taarifa ya Haki za Binadamu Kimataifa ya Microsoft

Kukokotoa, uvumbuzi unaendeshwa kidijitali na muunganisho ni baadhi ya nguvu zenye ushawishi mkubwa kazini leo. Ni msingi wa shughuli za biashara za Microsoft na tunaziona zikibadilisha maisha ya watu kila mahali. Kwa kuwa na msingi wa kanuni iliyotangazwa katika Azimio la Kilimwengu la Haki za Binadamu kwamba "watu wote wamezaliwa huru na sawa kwa hadhi na haki", tumeahidi kuunda teknolojia na huduma zinazoimarisha mtu na hali za pamoja kote ulimwenguni. Taarifa ya Haki za Binadamu Kimataifa ya Microsoft inaeleza mbinu yetu ya kuimarisha hadhi ya binadamu na kuheshimu haki za binadamu.

## Utangulizi

Teknolojia inapaswa kutumiwa kwa manufaa ya binadamu, kumwezesha na kumlinda kila mtu na kutomwacha yeyote nyuma. Kuheshimu haki za binadamu ni thamani ya msingi ya Microsoft Haiwezi kutenganishwa na madhumuni yetu ya kuwezesha kila mtu na kila shirika duniani kufanikisha mengi kwa kutumia teknolojia zetu. Tunaamini kuwa watu, mashirika na jamii zitatumia tu teknolojia zinazoziamini na zitaamnini tu teknolojia zinazoheshimu haki na  zao na kukuza hadhi ya binadamu, shirika na hali njema.

Ingawa kujali na heshima kwa wengine ni thamani msingi ya Microsoft, mbinu yetu ya kukuza haki za binadamu kote duniani inajumuisha sheria, kanuni na kaida za kimataifa, ikiwemo Azimio la Kilimwengu la Haki za Binadamu, Agano la Kimataifa kuhusu Haki za Raia na Siasa, Agano la Kimataifa kuhusu Haki za Uchumi, Jamii na Tamaduni na kazi ya Umoja wa Mataifa kuhusu uongozi bora na utawala wa sheria.

Microsoft imeahidi kuwasaidia watu kutumia teknolojia:

- Kwa ajili ya manufaa ya binadamu
- Kuungana na watu wengine duniani, kutapata na kushiriki taarifa, maarifa, hoja na msukumo
- Kukabiliana na ubaguzi, kutengwa au ukandamizaji
- Kuokoa sayari yetu
- Kuimarisha afya na hali njema ya watu kila mahali
- Kutetea na kukuza demokrasia, uongozi bora na utawala wa sheria
- Kulinda na kukuza faragha, usalama, ulinzi na uhuru wa maoni, kujieleza, kujumuika, mkutano wa amani na haki nyingine za binadamu

**Jinsi tunavyotimiza ahadi hii:**

- Kushirikisha, kujifunza kutoka kwa na kufanya kazi na wadau mbalimbali: Ushirikishaji huleta mazungumzo. Mazungumzo huturuhusu kushiriki thamani zetu, sauti yetu na maarifa yetu ya teknolojia zinazoibuka mara kwa mara na jinsi zinavyoweza na zinavyopaswa kutumiwa. Hutusaidia kujifunza na kuelewa hoja na mitazamo ya wadau kutoka sehemu zote za jamii duniani kote. Tunashirikiana nao kupata hoja na masuluhisho ya jamii ya dijitali inayoheshimu na kukuza haki za binadamu.
- Kumbatia changamoto na kufanya na kuzungumzia kile ambacho ni sahihi: Tunaamini tunaweza kuheshimu haki za binadamu kwa ufanisi zaidi wa kuwepo, badala ya kutokuwepo kwenye nchi zilizo na changamoto kubwa sana za haki za binadamu. Tunaamini kuwa mwishowe, kushirikisha watu, serikali na wadau wengine kwa kuwajibika katika mazingira magumu mara nyingi huleta ahadi bora za kukuza haki za binadamu.
- Kutekeleza haki za binadamu katika biashara na teknolojia zetu: Tunafanya uchunguzi wa kina ili kutathmini athari ya teknolojia zetu kwenye haki za binadamu. Tunazingatia kanuni na kaida za kimataifa kama vile Kanuni za Kuongoza za Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Biashara na Binadamu ili kuongoza jitihada zetu. Tunatumia kile tunachojifunza kutoka kwa wadau ili kuzipa changamoto fikira zetu, kuunda na kuboresha sera na desturi zetu, kupunguza hatari na kuimarisha teknolojia zetu na jinsi tunavyozitoa ili kutimiza ahadi yetu kuhusu haki za binadamu.



Brad Smith, Rais

## Jukumu letu

Teknolojia inaendelea kuwa njia msingi ya kutekeleza haki za binadamu kila mahali. Kama kampuni ya teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) ya kimataifa, tuna jukumu la kuwa kuna mustakabali endelevu ambapo kila mtu anaweza kufikia manufaa yanayotokana na teknolojia. Tunajitahidi kuunda bidhaa na kutoa huduma zinazostahiki kuaminika na kuthaminiwa na wateja kote duniani. Kuanza na muundo na maendeleo ya bidhaa yetu hadi utengenezaji na udhibiti wa mfumo wa ugavi na hatimaye usambazaji – tunajitahidi kutambua na kuelewa athari chanya na mbaya za haki za binadamu.

Ili kutusaidia kudhibiti jitihada hizi Microsoft inaahidi kuheshimu Kanuni za Kuongoza za Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Biashara na Binadamu (UNGPs). Tunajitahidi kila siku kutekeleza UNGP kwenye Microsoft nzima, kwenye makao makuu na ofisi zilizo katika takribani nchi na himaya 200 na kwenye mifumo yetu yote ya ugavi kimataifa.

UNGP zinaziomba biashara kuheshimu haki za binadamu kwa kufanya uchunguzi wa kina kuhusu jinsi shughuli zazo zinavyoweza kuathiri vibaya haki za binadamu, kupunguza athari mbaya na kusuluhisha madhara. Tunawafahamisha wadau ahadi yetu kupitia tovuti ya Taarifa ya Haki za Binadamu ya Kimataifa ambapo taarifa hii inapatikana kwa lugha na lahaja 18.

**Kufafanua haki za binadamu:** Kama kampuni ya teknolojia kimataifa yenye wadau wa haki kote duniani tunaahidi kuheshimu haki zote za binadamu – raia, siasa, uchumi, jamii na tamaduni. Haswa, Microsoft imeahidi kuheshimu haki za binadamu chini ya sheria zifuatazo za haki za binadamu kimataifa:

- Azimio la Kilimwengu la Haki za Binadamu
- Agano la Kimataifa kuhusu Haki za Raia na Siasa
- Agano la Kimataifa kuhusu Haki za Uchumi, Jamii na Tamaduni
- Azimio la Shirika la Wafanyakazi Kimataifa kuhusu Kanuni na Haki Msingi Kazini
- Mapatano kuhusu Uondoaji wa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake
- Mapatano kuhusu Haki za Mtoto
- Mapatano kuhusu Haki za Watu walio na Ulemavu
- Mapatano ya Kimataifa kuhusu Uondoaji wa Aina Zote za Ubaguzi wa Rangi
- Mapatano ya Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Haki za Wafanyakazi Wote Wahamiaji na Wanafamilia Wao
- Mapatano ya Geneva na Itifaki zao za Ziada
- Amri ya Roma ya Mahakama ya Uhalifu ya Kimataifa
- Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji
- Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu

Pia sisi ni wanachama, au waweka sahihi wa mifumo na mikakati ya wadau mbalimbali ifuatayo:

- Haki za Watoto na Kanuni za Biashara
- Mkakati wa Mtandao wa Kimataifa
- Malengo ya Maendeleo Endelevu
- Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa
- Viwango vya Umoja wa Mataifa vya Maadili ya Biashara kuhusu Kukabiliana na Ubaguzi dhidi ya wana LGBTI
- Kanuni za Kuwawezesha Wanawake

## Kanuni za msingi

Mbinu yetu inategemea kanuni zifuatazo:

**Ahadi yetu kwa uchunguzi wa kina unaoendelea kuhusu haki za binadamu:** Kuelewa athari zinazotarajiwa za haki za binadamu ambazo zinahusishwa na teknolojia za dijitali kunaibua changamoto za kipekee. Michakato yetu ya kimataifa na inayoendelea huanza kwa kulenga kutambua na kutathmini athari yoyote halisi, inayotarajiwa au mbaya ya haki za binadamu tunayoweza kusababisha, kuchangia au kuhusishwa moja kwa moja nayo, kupitia shughuli zetu binafsi au kutokana na mahusiano yetu ya biashara. Michakato yetu hufuata Miongozo ya UNGP na OECD ya Biashara za Kimataifa. Moja ya njia tunazofanya tathmini za athari za haki za binadamu (HRIAs), kutambua na kuzipa kipaumbele hatari kubwa. Tumefanya HRIA kwenye ngazi za shirika na bidhaa na kwa nchi na maeneo mbalimbali. Kazi yetu ya HRIA inajumuisha ushirikishaji wa mara kwa mara na kushauriana na wadau katika jitihada ya kuelewa na kuangazia mitazamo ya makundi au watu walio hatarini.

Wakati tathmini imekamilika, tunajumuisha na kuangazia matokeo yetu na kufuatilia utekelezaji kwenye kampuni nzima na muda wa bidhaa. Tunawasiliana na wadau jinsi athari chanya na mbaya zinavyotambuliwa, kutathminiwa na kuchukuliwa hatua kupitia ripoti yetu ya CSR inayoendelea, ripoti za kila mwaka za haki za binadamu, Ripoti za Digital Trust za Kila Miaka Miwilina mifumo mingine. Tunajitahidi kuelewa na kujibu kwa ufanisi hatari zinazoibuka, desturi bora na mahitaji ya wadau.

**Ahadi yetu ya suluhisho:** Suluhisho ni sehemu kuu ya jukumu la shirka kuheshimu haki za binadamu na tumeahidi kutoa mbinu fanifu za manung`uniko na ufikiaji wa suluhisho katika hali ambapo Microsoft huenda imesababisha au kuchangia athari mbaya za haki za binadamu. Tunaahidi kutozuia mifumo ya manung`uniko wala masuluhisho yaliyowezeshwa ili kufikiwa au kutolewa na wengine, ikiwemo Majimbo. Tumeahidi kujihusisha katika ushirikiano unaoendelea wa mikakati ya suluhisho kwenye shughuli zetu zote za biashara, ikiwemo wagawaji wa wetu wa ICT. Tunajitahidi kuhakikisha kuwa wenye haki wote na wawakilishi wao wanafahamu haki zao kwenye mifumo hii. Tunatafsiri mwongozo wa suluhisho katika lugha mbalimbali ili kuhakikisha ufikiaji kwa wahusika walioathiriwa. Microsoft inapiga marufuku aina yoyote ya kisasi dhidi ya yeyote anayeibua malalamishi au swali linalohusiana na haki za binadamu au kushiriki katika uchunguzi unaofuata wa malalamishi yoyote kama hayo.

Yeyote anayetaka kuibua manung`uniko au kutafuta suluhisho kutoka kwa Microsoft kuhusu utendakazi wetu wa haki za binadamu anaweza kufanya hivyo kwa njia za siri zifuatazo, kwa lugha nyingi:

- Wasilisha ripoti isiyotambulisha mtu kupitia Tovuti ya Microsoft Integrity
- Tuma barua pepe kwa Anwani ya Barua pepe ya Microsoft Business Conduct
- Piga simu ya Dharura ya bila malipo ya Microsoft Integrity

Pia tunatoa mifumo ya bidhaa mahususi kwa ajili ya kuwasilisha hoja mahususi, ikiwemo:

- Ufikiaji: Disability Answer Desk na Enterprise Disability Answer Desk hutoa usaidizi kwa watu na mashirika yaliyo na maswali kuhusu ufikiaji wa bidhaa na huduma za Microsoft.
- Michezo: Xbox Live Policy & Enforcement inadumisha na kukuza hali salama na inayofurahisha kwa washiriki wote wa Xbox Live Platform and Community.
- Faragha: Fomu ya Usaidizi wa Faragha inatoa nafasi na kuibua maswali kuhusu desturi za faragha za Microsoft na kuomba haki za mhusika wa data kama vile haki ya kufikia na kufuta data binafsi.
- Jukumu la Mfumo wa Ugawaji wa Vifaa: Workers' Voice Hotline Program huwapa wafanyakazi wa kiwanda mfumo wa kuripoti wa kuaminika na usiotambulisha unaodhibitiwa na mtoa huduma mwingine asiyeegemea upande wowote.

**Ahadi yetu ya kuunga mkono uongozi bora na utawala wa sheria**: Uwezo wa Microsoft kuheshimu haki za binadamu unawezeshwa na uongozi bora na utawala wa sheria kote duniani Uongozi bora na utawala wa sheria unahitaji michakato ya wazi, ya kuwajibika, kujukumika na shirikishi inayoshughulikia mahitaji na matamanio ya watu na jamii. Uongozi bora na utawala wa sheria unahusiana kwa karibu na kazi safi, maisha endelevu, usalama wa watu na uhuru wao wa serikali kutokiuka haki zao za binadamu.

Tunatetea sera na sheria za umma zinazoendeleza uvumbuzi huku zikilinda haki za binadamu. Tunafanya hili kupitia ushirikishaji wa wadau mbalimbali wa mataifa, kanda na eneo.

Kama kampuni ya kimataifa inayopigia debe utawala wa sheria, tunajua kuwa hatuko juu ua sheria. Tunaheshimu sheria za taifa zinazotumika. Lakini sheria ya taifa ni msingi tu. Pale ambapo viwango vya kimataifa vya haki za binadamu vinazidi sheria za taifa, tunatetea utambuaji wa kisheria wa kaida za kimataifa na kujitahidi kuweka desturi na shughuli za biashara zetu kulingana na viwango vya kimataifa.

**Ahadi yetu ya ushirikishaji**: Tunaamini kuwa ushirikishaji wa kuwajibika na watu na serikali katika nchi zenye changamoto kubwa za haki za binadamu mara nyingi huwa na ahadi kubwa zaidi ya ukuaji wa haki; mara nyingi tunaweza kutimiza kwa ufanisi zaidi ahadi zetu za haki za binadamu za kimataifa kupitia uwepo, badala ya kutokuwepo katika nchi kama hizo.

Tunatambua kuwa mazingira kama hayo ya kufanyia kazi yanahitaji uchunguzi wa kina zaidi na utii wa kanuni bayana. Tumejitolea kuelewa jinsi miktadha hii inavyoweza kuongeza hatari ya athari mbaya za haki za binadamu na jinsi tunavyoweza kuzuia au kupunguza athari kama hizo. Mambo muhimu ya kufaulisha mbinu hii ni pamoja na matumizi ya ushirikishaji na ushauri wa wadau mbalimbali, ikiwemo makundi ya wadau wa ndani na kutumia sifa, sauti na maamuzi mbalimbali ya biashara yetu kuwashawishi wadau wengine msingi.

**Ahadi yetu kwa makundi yaliyo hatarini:** Ingawa haki za binadamu ni za kilimwengu, hazifurahiwi kilimwengu. Kwa mfano, aina mbalimbali za ubaguzi zinahitaji tuzingatie mahususi makundi yaliyo hatarini. Makundi yaliyo hatarini ni pamoja na watu walio na uwezekano wa kuathiriwa vibaya, au walio na ufikiaji mdogo wa suluhisho. Tumeahidi kufanya biashara bila ubaguzi kwa msingi wa mbari, rangi, kabila, jinsia, lugha, dini, siasa au maoni, asili ya taifa au jamii, mali, hali ya kuzaliwa au nyingine kama vile ulemavu, umri, hadhi ya ndoa na familia, jinsia, mwelekeo wa ngono, utambulisho wa jinsia, hali ya afya, makazi, hali ya uchumi na jamii, au sifa nyingine au aina nyingi za ubaguzi zinazoshawishi utimizaji wa haki za binadamu. Tunaahidi kuchukua hatua ili kuwezesha makundi yaliyo hatarini kutekeleza haki zao vizuri.

**Ahadi yetu kwa watetezi wa haki za binadamu**: Ahadi yetu ya kuheshimu na kukuza haki za binadamu ni pamoja na heshima na usaidizi wa kazi ya watetezi wa haki za binadamu kote duniani. Watetezi wa haki za binadamu ni watu binafsi au pamoja na wengine, wanashiriki katika shughuli na utetezi unaochangia kwenye ulinzi wa haki za binadamu na utawala wa sheria, uongozi bora, stahamala na utofauti na ujumuishaji. Watetezi wa haki za binadamu wanakabiliwa na vitisho endelevu vya mwili, jamii, uchumi na saikolojia. Microsoft haikubali vitisho, kisasi, shambulio la mwili, sheria wala mtandaoni dhidi ya watetezi wa haki za binadamu. Ahadi hii inawahusu pia watetezi wote wa haki za binadamu, ikiwemo wale wanaoshughulikia masuala yanayohusiana na Microsoft na wale wanaotekeleza haki zao za uhuru wa kujieleza, mwungano na kukusanyika kwa amani, ikiwemo kupinga au kukataa vipengele vya biashara yetu binafsi.

Katika nchi zote na haswa katika zile zilizo na ulinzi dhaifu wa uhuru wa raia na ambao vitisho kwa watetezi wa haki za binadamu vinasemwa sana, tunaahidi kushauriana na watezi wetu wa haki za binadamu kama sehemu ya uchunguzi wetu wa kina wa haki za binadamu na kusaidia kazi yao yenye ongezeko la mabadiliko kwenye changamoto na magumu wanayokumbana nayo. Tunajitahidi kujenga uwezo wa watetezi wa haki za binadamu kufanikisha malengo yao kupitia uaminifu ulioongezeka katika teknolojia. Ili kufanikisha lengo hilo Microsoft pia inaahidi kuwezesha na kukuza usalama wa mtandaoni wa watetezi wa haki za binadamu na matumzi yao ya teknolojia.

**Ahadi yetu ya kupunguza mabadiliko ya tabianchi:** Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha changamoto ya ajira kamili ya haki nyingi za binadamu na kuzidisha umaskini wa sasa na kukosekana kwa usawa. Hatuwezi kutimiza majukumu yetu ya haki za binadamu katika dunia iliyoathiriwa vibaya na mabadiliko ya tabianchi. Ahadi yetu  ya kupunguza mabadiliko ya tabianchi inalenga kaboni, mifumo ya ikolojia, maji na taka na inatekelezwa kwenye shughuli zetu zote na mfumo wa ugawaji. Tunaheshimu haki ya ardhi, maliasili na maji. Tunatambua jukumu letu la kudhibiti athari za mazingira na uchumi za ofisi zetu, wagawaji wetu na wazalishaji wa malighafi, zinazoweza kuwa na athari nzuri na mbaya kwenye ustawi wa kifedha wa watu binafsi na familia. Tunafuatilia na kuripoti kuhusu maendeleo yetu ya malengo endelevu ya mazingira ya 2030 katika ripoti ya mazingira endelevu.

Tunatambua kuwa makundi na jamii nyingine ziko kwenye hatari sana kuliko nyingine kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi, ikiwemo wanawake, jamii zinazoishi kwenye au karibu na umaskini, wenyeji na makundi yaliyotengwa. Uelewa wetu wa hatari hizi unachochea mbinu yetu ya mpito wa haki na haki ya tabia nchi. Tunaahidi kushirikisha jamii zilizotengwa, au wawakilishi wao halali, wakati wa kuunda sera na desturi zetu endelevu. Tunaahidi kutumia teknolojia na uvumbuzi wetu kusaidia jamii zilizo hatarini kukuza uthabiti wao wa tabia nchi.

**Ahadi yetu kwa ushirikiano nah atua ya pamoja**: Changamoto chache za haki za binadamu zinazohusiana na teknolojia za dijitali zinaweza kushughulikiwa kupitia kampuni moja, au hata tasnia moja inayohudumu peke yake, hivyo ushirika na ushirikiano wa wadau mbalimbali ni msingi wa jitihada zetu.

Tulikuwa watia sahihi wa mwanzo kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa na nisi ni waanzilishi wa Global Network Initiative (GNI), jitihada ya pamoja miongoni mwa kampuni za ICT, mashirika ya jamii, wawekezaji wanaowajibika kijamii na masomo. Tunaahidi kutii Kanuni za GNI kuhusu uhuru wa kujieleza na haki za faragha.

Tunatambua vitisho kwenye michakato yetu ya demokrasia kutokana na uzuiaji uliowezeshwa na mtandao na tunashirikiana na wadau ikiwemo serikali, mashirika yasiyo ya serikali, vyuo, na tasnia kimataifa ili kulinda kampeni za kisiasa dhidi ya udukizaji, kuongeza uwazi unaohusiana na matangazo ya siasa mtandaoni, kuchunguza masuluhisho ya teknolojia ili kuhifadhi na kulinda michakato ya kura na kutetea dhidi ya kampeni za habari za kupotosha.

Pia tunashirikiana na wengine katika tasnia – huku pia tukishauriana na mashirika ya jamii,watafiti, serikali na wakala wa kutekeleza sheria kote duniani – kupambana na dhuluma za mifumo ya dijitali. Kwa mfano, tunashiriki kikamilifu katika Global Internet Forum to Counter Terrorism (GIFCT) na WePROTECT Global Alliance to End Child Exploitation Online. Kwa kuzingatia ahadi yetu ya bidhaa na huduma za teknolojia zinaweza kufikiwa, tunashiriki kikamilifu katika Global Initiative for Inclusive ICTs (G3ict).

Nje ya sekta ya teknolojia, sisi ni watia sahihi wa Joint Labor Union and CEO Statement kwenye Makubaliano ya Paris, tukiahidi mpito wa haki wa wafanyakazi uliopatikana kupitia mazungumzo na wafanyakazi na miungano yao. Tunajitahidi kuwezesha mashirika yanayofanya utafiti wa mabadiliko ya tabianchi na kuyaimarisha. Tunatumia sauti yetu kuzungumza kuhusu masuala ya sera ya umma yatakayokuwa muhimu kwa upunguzaji wa athari ya kaboni kwa binadamu na kudhibiti mifumo ya ikolojia. Kwa kushirikisha kampuni kwenye tansia zote ili kushiriki jinsi tunavyotekeleza ahadi zetu za haki za binadamu, tunatamani kutumika kama kichocheo cha hatua na wengine katika sekta ya teknolojia na zaidi.

## Sehemu muhimu za athari

Microsoft inaweza kutimiza vyema jukumu lake la kuheshimu haki za binadamu kupitia kazi yetu katika sehemu tano muhimu:

**Sera na desturi zetu kuhusu madai ya serikali**: Ahadi yetu ya utawala wa sheria inahusu jukumu la kisheria la kutii sheria ya ndani inayotumika. Tunapokabiliwa na maombi kutoka kwa serikali kutoa data ya mtumiaji au kuondoa maudhui, tunajitahidi kuheshimu haki za binadamu za faragha na uhuru wa kujieleza kwa kutathmini ikiwa maombi ya serikali ni halali, yanabana kisheria, yanatii sheria inayotumika na yanalingana na sheria ya kimataifa na kaida za haki za binadamu kimataifa.

**Wateja wetu**: Kama thibitisho la ahadi yetu kwa haki za binadamu na kwa mabilioni ya watumiaji kote ulimwenguni, tunajitahidi kupunguza na kuzuia hatari kwa kutumia ufanyaji maamuzi ya kuhamasisha kuhusu haki muda wote wa bidhaa na mahusiano ya biashara yetu. Kwa mfano, tumeahidi utashi wa kompyuta (AI) wa kuwajibika kwa kutumia kanuni zetu za AI kwenye maendeleo na matumizi yake. Tunaupa kipaumbele ufikiaji kwa kutumia kanuni zetu jumuishi za muundo ili kutimiza ahadi yetu ya kuunda na kutoa teknolojia inayowezesha watu walio na ulemavu. Kwa haki ya binadamu ya faragha tunatumia kanuni zetu za faragha kuwezesha wateja wetu kudhibiti data zao na kutoa mbinu mahususi ya manung`uniko kwa hoja wanazoweza kuwa nazo. Pia tunatumia hatua ya pamoja kusaidia kuzuia na kuangazia baadhi ya madhara yanayoweza kutokea ya bidhaa zetu ambayo wengi wetu katika tasnia ya teknolojia tunakumbana nayo.

**Waajiriwa wetu**: Tunaahidi kuheshimu haki za waajiriwa wetu, ikiwemo zile zilizobainishwa katika Azimio la ILO kuhusu Kanuni na Haki za Msingi Kazini: Uhuru wao wa muungano na haki ya makubaliano ya pamoja, haki zao za kutopewa kazi ya kushurutisha, ajira kwa watoto au ubaguzi kuhusu ajira na kazi. Ili kuendeleza utamaduni wa kweli wa utofauti na ujumuishaji katika mahali pa kazi, tumeahidi

kupangilia desturi zetu na Mkataba kuhusu Uondoaji wa Ubaguzi Dhidi ya Wanawake, Mkataba kuhusu Haki za Watu walio na Ulemavu na Viwango vya Umoja wa Mataifa kuhusu Baadili ya Biashara Inayopambana na Ubaguzi dhidi ya wana LGBTI. Sera zetu zinazojumuisha ahadi hizi ni pamoja na Sera ya Nafasi Sawa ya Ajira, Sera ya Kupambana na Ubaguzi na Unyanysajina Viwango vyetu vya Maadili ya Biashara. Sera hizi zinakamilishwa na mipango mbalimbali inayosaidia hali njema ya waajiriwa wetu na wanafamilia wao.

**Wagawaji wetu**: Kazi safi ni muhimu kwa maisha jumuihi na endelevu na ni msingi wa maisha ya hadhi. Tunajitahidi kukakikisha kuwa kila mtu anayetengeneza bidhaa zetu anaheshimiwa na kupewa hadhi. Microsoft inawatarajia wagawaji wake kuzingatia kikamilifu sheria za ajira, kushiriki ahadi yake ya kuheshimu haki zote za binadamu na kutoa nafasi sawa mahali pa kazi na kuchukua hatua zinazofaa kusuluhisha athari zozote mbaya za haki za binadamu.

Microsoft ina mahusiano na maelfu ya wagawaji kote ulimwenguni. Ili kuboresha malengo yetu ya jukumu la mfumo wa ugawaji, tunawekeza sana katika mahusiano ya wagawaji wetu na ahadi yaetu ya haki za binadamu inahusu pia wagawaji wetu wote. Tunawatarajia wagawaji wetu wote wanaofanya biashara na Microsoft kutekeleza haki za binadamu, desturi za ajira, afya na usalama, mazingira na maadili zilizoelezwa katika Kanuni ya Maadili ya Wagawaji (SCoc) na wagawaji wa maunzi, Microsoft Supplier Social and Environmental Accountability Manual (Suppliers SEA Manual).

SCoC, Supplier SEA Manual na mipango yetu mipana ya jukumu la mfumo wa ugawaji yote hufuata Azimio la ILO kuhusu Kanuni na Haki za Msingi Kazini, mikataba Msingi ya ILO, vipengele husika vya Mkataba kuhusu Haki za Mtoto, Mkataba kuhusu Uondoaji wa Ubaguzi Dhidi ya Wanawake, Mkataba kuhusu Haki za Watu walio na Ulemavu na Viwango vya Umoja wa Mataifa kuhusu Baadili ya Biashara Inayopambana na Ubaguzi dhidi ya wana LGBTI. Isitoshe, SCoC ni chombo chetu muhimu cha kuzuia utumwa wa kisasa na ulanguzi wa watu katika mifumo yetu ya ugawaji kimataifa, ikiwemo kuheshimu saa za kufanya kazi, uhuru wa mwungano na miongozo ya makubaliano ya pamoja iliyowekwa na mikataba ya msingi ya ILO.

Tumeahidi kuondoa ulanguzi wa watu na ajira za kushurutisha kwenye mfumo wetu wa ugawaji, ikiwemo miongoni mwa wafanyakazi wetu wa ziada. Tunaelewa kuwa wafnayakazi wa wahamiaji wa kigeni (FMWs) wako kwenye hatari ya ajira ya kushurutisha na tumeahidi kuheshimu Mkataba kuhusu Ulinzi wa Haki za Wafanyakazi Wote Wahamiaji na Wanafamilia Wao. Ahadi yetu ya kuondoa ulanguzi wa watu kwenye mfumo wetu wa ugawaji imekita kwenye SCoC na itifaki zetu za mpango wa jukumu la mfumo. Tunakiri kuwa kushughulikia matatizo makuu zaidi ya haki za binadamu katika mfumo tata wa ugawaji ni jukumu la pamoja, mara nyingi linalohitaji mbinu pana za tasnia na wadaua mbalimbali. Kwa hivyo, tunashiriki katika Muungano wa Biashara ya Uwajibikaji, Mkakati wa Madini wa Kuwajibika, Mkakati wa Hakikisho la Uchimbaji Migodi wa Kuwajibika, Teknolojia Dhidi ya Ulanguzina Mwungano wa Biashara za Kimataifa Dhidi ya Ulanguzi wa Watu.

Tunajali sana kuhusu uendelevu wa mfumo wetu wa ugawaji wa malighafi. Microsoft haivuni wala kuzalisha malighafi, lakini tunawashawishi uvunaji na uzalishaji wa malaghafi kupitia sera na desturi

zetu. Kwa Vifaa vyetu, mbinu yetu kwa malighafi huanza na Sera ya Microsoft Responsible Sourcing of Raw Materials (RSRM) Policy. Sera ya RSRM inapanua Kanuni yetu ya Maadili ya Wagawaji hadi umbali wa mfumo wetu wa ugawaji wa malighafi kwa kuunga mkono haki z abinadmau, ajira, afya na usalama, ulinzi wa mazingira na maadili ya biashara. Sera hii inashughulikia madini na nyenzo zote zilizotumiwa katika maunzi ya Vifaa vyetu na mfumo wa ugawaji wa vifurushi, pasipo mpaka wa jiografia.

**Jamii zetu**: Tuwe jamii tajiri kupitia shughuli zetu au mfumo wa ugawaji, au kupitia matumizi ya teknolojia zetu, Microsoft inatambua kwamba tunawaathiri wenye haki. Tunazingatia athari zetu zinazoweza kutokea na halisi za haki za binadamu kwenye jamii tunazofikia katika michakato yetu ya uchunguzi wa kina. Pia tunawekeza katika nafasi mahususi ili kukuza haki za jamii zetu za ndani na ulimwenguni kupitia msaada wa binadamu na michango isiyo ya faida.

Kupitia Microsoft Philanthropies, tunachanga na kupunguza bei ya bidhaa za uzalishaji, mfumo na teknolojia ya wingu ili kuwezesha mashirika yasiyo ya faida kote ulimwenguni kuchangia mabadiliko makubwa kwenye jamii wanazotumikia. Kwa kutoa huduma zetu za wingu na programu bila malipo au kwa punguzo kubwa kwa mashirika yasiyo ya faida yanayostahiki, tunawezesha mashirika ya haki za binadamu kote duniani kuimarisha dhamira zayo. Tunashirikiana na mashirika yasiyo ya faida kutoa rasilimali na mafunzo ya stadi za dijitali kwa watu waliopoteza makao, kuwawezesha kwa ufikiaji wa nafasi za elimu na uchumi. Wakati wa janga hatari kwa binadamu, tunasaidia jamii zilizoathiriwa kufikia teknolojia na taarifa wakati na mahali zinazihitaji sana. Tunajitahidi kusaidia mashirika kuongeza utayari na kutangulia kutoa usaidizi huku ykiboresha uwezo wao wa kukabiliana na majanga ya baadaye.

Ili kusaidia kutimiza dhamira yetu, Microsoft imejitolea kuimarisha dunia jumuishi na yenye usawa zaidi. Tumeahidi kuziba pengo la nafasi ambayo vijana wengi wanakabiliwa nayo leo kupitia uwekezaji wetu katika jamii, kulenga stadi za uwezekano wa kupata ajira na ufikiaji wa mtandao wa bei nafuu katika jamii zenye huduma na uwakilishi wa kiwango cha chini. Kupitia mpango wa Microsoft Employee Giving waajiriwa wetu hutenga muda, vipaji na pesa zao na kuyapa mashirika yasiyo ya faida wanayotaka, pamoja na fedha zinazolingana ambazo zinatolewa na kampuni.

## Uongozi wa ndani

Waajiriwa, wabia, wagawaji, serikali na wateja hushiriki jukumu hili ili kuhakikisha kuwa teknolojia ya habari na mawasiliano na shughuli za biashara yetu zinaheshimu na kukuza haki za binadamu.

Kamati ya Udhibiti na Sera ya Umma ya Bodi ya Wakurugenzi ya Microsoft husimamia hatari msingi za udhibiti usio wa fedha zinazoweza kuwa na athari ya nyenzo kwenye kampuni na uwezo wake wa kudumisha uaminifu kwa wateja, waajiriwa na umma. Hii ni pamoja na sera na mipango inayohusu masuala ya sheria, udhibiti na uzingatiaji yanayohusiana na ushindani na kupigana na uaminifu, faragha, biashara, usalama wa dijitali, utashi wa kompyuta na uendelevu wa mazingira na pia masuala makubwa yanayohusiana na ufikiaji, haki za binadamu na jukumu la mfumo wa ugawaji. Kamati pia hupitia shughuli za mahusiano ya serikali na kampuni na shughuli za siasa na matumizi, ajenda ya sera ya umma na msimamo kuhusu masuala muhimu ya sera ya umma.

Rais na Afisa Mkuu wa Sheria wa Microsoft husimamia utekelezaji wa ahadi zetu za haki za binadamu ndani ya kitengo cha Masuala ya Shirika, Nje na ya Sheria ya Microsoft. Kitengo kina zaidi ya wataalamu 1,500 wa masuala ya biashara, sheria na shirika walio katika nchi 54 na wanaofanya kazi katika zaidi ya mataifa 120 kuhusu masuala mbalimbali yanayojumuisha uunganishaji baina ya teknolojia na jamii, ikiwemo usalama wa mtandaoni, faragha, maadili, utashi wa kompyuta, haki za binadmau, uhamiaji, uhisani na uendelevu wa mazingira.

Kituo cha Teknolojia na Haki za Binadamu cha Microsoft kilianzishwa 2013 na huangazia na kuratibu uchunguzi wetu wa kina wa haki za binadamu, hutambua hatari na nafasi zinazoibuka ambazo zinahusiana na haki za binadamu. Kituo kinakuza mbinu zilizopatanishwa za haki za binadamu kwenye kampuni nzima na kuhimiza mazungumzo ili kuimarisha uelewa wa athari za haki za binadamu za ICT. Kupitia Kituo, Microsoft hushirikisha na kushauriana na makundi ya haki za binadamu, vyuo na makundi ya tasnia mbalimbali ulimwenguni ili kushiriki hali na mafunzo ya Microsoft waliyojifunza.